JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ILEJE

SHULE YA SEKONDARI KAFULE,
S.L.P 09,
ILEJE-SONGWE
……../……../2018

SIMU NO.0768332311-Mkuu wa shule
0757718232-Makamu
0769030831-Matron
0759699746-Patron

KUMB.NA.KSS/F/V/VOL,I/

MZAZI/MLEZI WA----------

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KAFULE KIDATO CHA TANO JULY-2018 (JOINING INSTRUCTIONS)

Ninafurahi kukuarifu kuwa mtoto wako---------- Amechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari kafule kuanza kidato cha tano HGK,HGL.Napenda kutumia fursa hii kumpongeza mwanao kwa juhudi kubwa alizoonesha katika masomo akiwa kidato cha kwanza hadi cha nne.Kama angelegea asingepata nafasi hii.

MAHALI ILIPO SHULE

Shule ya sekondari kafule iko mkoani songwe (mkoa wa zamani Mbeya),wilayani Ileje,km 63 toka makao makuu ya wilaya karibu na hospitali ya wilaya inayoitwa Isoko.Ukitoka mbeya panda magari yanayoenda Tunduma,shuka Mpemba,ukitoka DSM panda magari yanayokwenda Tunduma au Sumbawanga na ushuke Mpemba,kadhalika kama unatoka njia ya Sumbawanga,panda magari yanayokwenda Mbeya kisha shuka Mpemba (baada ya kupita Tunduma)

Toka Mpemba utapata magari yanayokwenda isoko yapo magari makubwa na madogo pia.Ni vema ukifika mpemba saa 5:00 asubuhi,utapata kwa urahisi magari yanayokwenda Isoko.Mjulishe kondakta kuwa ni mwanafunzi unayekwenda kafule sekondari naye atakushushia stendi sahihi.Shule itafunguliwa rasmi tarehe……/……../2018 na mwanafunzi anatakiwa kufika siku hiyo tangu saa 3:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni.

Mwanafunzi atapokelewa kama atakuwa:-

i) Amejaza kwa usahihi fomu ya kukubali kujiunga na shule hii akishirikiana na mzazi/mlezi wake.
ii) Amepimwa afya yake katika hospitali/kituo cha afya na fomu ya request for medical examination imejazwa na medical officer (katika hospitali/kituo cha afya cha serikali)
iii) Amejaza kwa usahihi taarifa binafsi na kwa uaminifu
iv) Amekamilisha maagizo yote yaliyoandikwa katika barua hii na mahitaji ya lazima ya shule (karo na michango mingine) form namba 1-1V zimeambatanishwa na barua hii.

Baada ya kukamilisha maagizo yote hapo juu,mwanafunzi aje na fomu(zilizojazwa) siku ya kwanza.Asipokuja nazo HAPOKELEWI (HATAPOKELEWA)

Mwanafunzi anatakiwa afike hapa shuleni mapema (tarehe ya kufunguliwa)asije akapoteza nafasi yake.Kama ameshindwa kufika au ameamua kutojiunga na shule hii anatakiwa atoe taarifa ya maandishi mapema kabla ya siku 30 tangu tarehe ya kungua shule.

Barua hiyo itumwe kwa

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI KAFULE,
S.L.P 09,
ILEJE.-SONGWE. SIMU 0768332311.

<u>MAHITAJI YA SHULE</u>.

i) Ada ya shule kwa mwaka Tsh 70,000/= au 35000/= kwa muhula
ii) Michango mingine
   a) Fedha za taaluma Tsh elfu kumi (20000/-) elfu ishirini kwa mwaka
   b) Fedha za kitambulisho elfu tano tu (6000/-) elfu sita
   c) Fedha za ukarabati wa samani Tsh elfu kumi na tano (15000/-)
   e) Rim moja ya karatasi A4 kwa mwaka.
   f) Fedha ya matibabu Tsh elfu kumi (10000) kwa mwaka. Tsh.5000/- kwa ajili ya huduma ya kwanza na Tsh.5000 kwa ajili ya bima ya afya (kwa wasio na kadi za bima ya afya)
   g) Fedha kwa ajili ya masomo ya muda wa jioni na mitihani maalumu Tsh elfu ishirini (20000) kwa mwaka
   h) Fedha ya tahadhari Tsh.5000/-
   i) Fedha ya kuwalipa wapishi,walinzi na vibarua wengine Tsh 30000/- kwa mwaka
   j) Fedha kwa ajili ya mock ya mkoa Tsh 20000/- kwa mwaka
   k) Fedha kwa ajili ya gharama za wino wa printer,photocopy na matengenezo Tsh 4000/- kwa mwaka

NB:Fedha zote zilipwe kwenye akaunti ya shule (**60801200063 NMB**) **<u>JINA LA ACCOUNT:</u> KAFULE SECONDARY SCHOOL RECURRENT EXPENDITURE** isipokua fedha za matibabu Tsh.10000/= Masomo ya muda wa jioni Tsh.20000/= fedha ya mtihani wa mock Tsh.20000/-

MUHIMU: 1. Hakikisha mwanafunzi anakuja na risiti za michango aliyolipia bank.
2**.** Mwanafunzi atapokelewa baada ya kukamilisha michango hiyo hapo juu.

SARE ZA SHULE

A: WAVULANA

i. Suruali moja rangi ya khaki na ya pili rangi ya bluu bahari pamoja na tai ndefu 2 za rangi blue bahari na khaki
ii. Mashati mawili(2) ya rangi nyeupe kitambaa cha tetroni yenye mikono mirefu na mfuko mmoja kifuani upande wa kushoto
iii. Sweta rangi ya kijani kibichi (kuna baridi ya wastani)
iv. Viatu vyeusi vya kamba kisigino kifupi jozi mbili na soksi nyeupe jozi mbili

B:WASICHANA

i. Sketi mbili(2) moja rangi ya khaki na ya pili rangi ya bluu bahari pamoja na tai ndefu 2 za rangi blue bahari na khaki
ii. Blauzi 2 za rangi nyeupe kitambaa cha tetroni yenye mikono mirefu na mfuko mmoja kifuani upande wa kushoto(Sample ya vitambaa vimeambatanishwa)

iii. Sweta ya rangi ya kijani kibichi (kuna baridi ya wastani)
iv. Viatu vyeusi vya kamba kisigino kifupi jozi mbili na soksi nyeupe jozi mbili

VITU VYA KUZINGATIA KWENYE SARE

Kwa wavulana:

i) Upana wa mkanda wa suruali kiuno uwe inchi 2
ii) Mifuko mitatu,miwili pembeni (wa kutoboa) nyuma mmoja upande wa kulia
iii) Upana wa suruali chini uwe inchi 17
iv) Suruali iwe na turnup na marinda mawili

Kwa wasichana:

i) Sketi iwe na urefu inchi 08 toka kwenye goti kwenda chini
ii) Upana wa marinda uwe inchi 3
iii) Zipu ikae upande wa kushoto wa sketi
iv) Upana wa mkanda wa kiunoni iwe inchi 2
v) Ziwe na mfuko mmoja upande wa kulia

SARE ZA MICHEZO

WAVULANA NA WASICHANA

- Bukta 2 rangi ya bluu
- Fulana 2 rangi ya bluu
- Viatu vya michezo raba jozi 2
- Soksi ndefu rangi nyekundu josi 2

RANGI YA HIJABU

Wanafunzi wa kike wa kiislamu watavaa hijabu rangi nyeupe.

NGUO ZA KUVAA BAADA YA VIPINDI VYA DARASANI NA SIKU ZA MAPUMZIKO

WASICHANA

- Truck suit bluu bahari
- Gauni la drafti nyeupe na bluu bahari lenye marinda ya kupanga
- T-shirt rangi ya kijivu

WAVULANA

- Truck suit rangi ya bluu bahari na mistari nyeupe
- Suruali rangi ya bluu mshono kama sare ya shule
- T-shirt yangi ya kijivu

MUHIMU:1. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na mavazi tofauti na hayo (masharti nje na hayo aliyoandikiwa katika barua yake ya kuitwa shuleni)

2. Maagizo ya mashono yaliyoagizwa yazingatiwe atakae kiuka maelekezo haya atachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunya ng'anywa mavazi hayo.

VIFAA VYA DARASANI

1. Counter book (Quire 4) tisa
2. Kalamu za wino na risasi za kutosha
3. Mkebe (mathematical set 1)

VIFAA VYA BWALONI NA BWENINI

1.Sahani,bakuli, kikombe na kijiko
2. Mswaki,sabuni, dawa ya mswaki,dawa ya viatu n.k
3.Godoro la futi 6 kwa inchi $2^{1}/_{2}$,blanketi 2,shuka 2 rangi ya bluu bahari,taulo,mto na folonya 2 za rangi ya shuka

i) Wasichana ndoo lita 10 (mbili),panga,soft broom,reki na mpini wake na squizer kwa ajiri ya usafi

ii) Wavulana ndoo lita 10 (mbili),panga,jembe lenye mpini na hard broom kwa ajiri ya usafi.Vifaa hivi vitapokelewa mara mwanafunzi anaporipoti.

MUHIMU:-Awe na sanduku la bati(Tranka) kwa ajiri ya kuhifadhia vifaa vyake.

USAJILI

Usajili utafanyika ofisini kwa makamu mkuu wa shule.Mwanafunzi atasajiliwa kwa kutumia jina lililoandikwa kwenye selform tu.Si ruhusa kubadilisha jina.Mwanafunzi atunze na kuikumbuka wakati wote namba yake ya usajili kipindi chote cha uanafunzi wake hapa shuleni.Atunze stakabadhi zote za malipo mbalimbali anayofanya shuleni na benki ili azioneshe kwa mtu yeyote anayehusika kwa ushahidi pindi utata unapojitokeza kuhusu malipo flani.

MUHIMU:1. Njoo na kadi ya matokeo yako ya kidato cha nne(result slip original na nakala yake) ''copy'' hata kama utatimiza masharti mengine bila result slip hutapokelewa.

2. Picha za paspotsize nne (4)

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria za shule za Elimu 25 ya mwaka 1978.Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na kupewa nakala yako mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi,wafanyakazi wote,wanafunzi wenzako na jamii kwa ujumla

b) Kila mwanafunzi lazima kuthamini na kuheshimu kazi zote

c) Kutimiza kwa makini maandalizi ya jioni(preparation)

d) Kuwahi katka kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa

e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu nya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wake katika shule hii

f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule

g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa

h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na kuhudhuria vipindi vyote kama ratiba ya darasa lako na ratiba akuu ya shule(daily routine)inavyoonesha.

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE MARA MOJA

1) Wizi
2) Uasherati,ubakaji na ushoga
3) Kunywa pombe,matumizi ya madawa ya kulevya
4) Uvutaji bangi/sigara
5) Makosa ya jinai
6) Kupigana,kupiga au kutumia lugha za matusi na kejeli
7) Kudharau Bendera ya Taifa
8) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
9) Kuoa au kuolewa
10) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
11) Kutoa mimba
12) Kugoma.kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule
13) Kukataa adhabu kwa makusudi
14) Kulala nje ya shule bila ruhusa ya MKUU WA SHULE

15) Kuwa na simu ya mkononi au laini,chaja,kamera,computa,radio,siraha au kitu chochote chenye ncha kali bwenini au darasani.

ZINGATIA:''***Matumizi ya simu kwa wanafunzi wawapo shuleni imekuwa ni tatizo kubwa sana,Mzazi/mlezi hakikisha unamsisitiza kijana wako kutokuja na simu wala kununua kwa kificho kwani itamsababisha afukuzwe shule itakapo bainika.''***

MAMBO MENGINE YA KUZINGATIA MWANAFUNZI AWAPO SHULENI:-

i) Mawasiliano yoyote kati ya mwanafunzi na mzazi au mlezi yatafanywa kupitia ofisi ya MKUU WA SHULE na namba za walezi zilizoorodheshwa hapo juu na si vinginevyo.Kamwe usiruhusu kijana wako kukupigia simu nje na namba ulizopewa kwenye barua hii.
j) Hairuhusiwi wanafunzi wa jinsia tofauti kutembea pamoja au kusimama pamoja kuongea katika mazingira yasiyo wazi au kukumbatiana katika mazingira yoyote.
k) Kutoka nje ya eneo la shule bila kuvaa sare ya shule wala kibali cha mwalimu wa zamu
l) Kutumia kwa umakini umeme,maji na kuzima switch au kufunga bomba la maji mara umalizapo matumizi.
m) Kutotembelea makazi ya walimu/wafanyakazi bila ruhusa toka kwa ,mwalimu wa zamu
n) Endapo utatembelewa na wazazi na mgeni yeyote mtambulishe kwanza mwalimu wa zamu kwa maelekezo zaidi.
o) Chakula kitaliwa ndani ya bwalo la chakula na si mahali pengine.Mwanafunzi hana ruhusa ya kuandaa chakula chake kando ya kinachoandaliwa na shule.Shule haiandai chakula cha pekee (special diet) mwanafunzi atakula kwa kufuata ratiba ya shule.
p) Wanafunzi wanaokwenda kuhudhuria ibada makanisani/msikitini wawe na kibali toka kwa mwalimu wa zamu/mkuun wa shule na saa 8:00 mchana awepo shuleni.Mwanafunzi hana ruhusa ya kushiriki mkesha wa aina yoyote.
q) Ni lazima mwanafunzi atii wito wowote unaotolewa na mwalimu/mtumishi na akimbie kuelekea unakotoka wito huo.Kengele ya wito inapogongwa ni wajibu wa mwanafunzi kukimbia kuelekea anakotakiwa kwenda.
r) Kila mwanafunzi anapaswa kuhudhuria Baraza la shule,Morning talk(speech) Morning parade,Afternoon parade,michezo,rolllcall zote.
s) Kwa kuwa shule ni mahali pa kupata elimu si ruhusa kwa mwanafunzi yeyote kupiga kelele darasani,maktaba,maabara na maeneo ya ofisi.n.k
t) Unapoondoka nyumbani hakikisha umechukua vifaa vyote vinavyohitajika darasani siku hiyo.Hutaruhusiwa kurudi nyumbani mara baada ya kufika shuleni.
u) Mwanafunzi wa kike haruhusiwi kusuka nywele awe na nywele fupi.

KWA WANAFUNZI WA BWENINI

i) Bweni litafungwa hadi wakati wa mapumziko/chakula
ii) Mazungumzo ya aina yoyote hayaruhusiwi baada ya saa 4:30 usiku hadi 11:30 asubuhi
iii) Ukaguzi wa siku (bed checking) utafanywa wakati wowote baada ya saa 4:00 usiku
iv) Siruhusa mgeni yeyote kuingia mabwenini,kadhalika wazazi hawaruhusiwi kuwatembelea watoto wao siku za masomo.Waweza kuwatembelea watoto wao

jumamosi ya nne ya kila mwezi saa 5:00 hadi saa 10:00 jioni.Mgeni apewe kibali na mwalimu wa zamu au mkuu wa shule.

v) Majina yanaitwa(Rollcall) saa 12:00 jioni kwa siku za sikukuu,jumamosi na jumapili.

vi) Siruhusa kwa mwanafunzi kulala bwenini wakati wa masomo au kazi za nje bila kibali cha daktari(matroni/patroni au mwalimu wa zamu)

vii) Baada ya masomo mwanafunzi wa bweni watatakiwa kuvaa:-

- Wasichana-Gauni la drafti nyeupe na bluu bahar, trucksuit bluu bahari na T-shirt ya kijivu
- Wavulana-Suruali ya bluu, T-shirt ya kijivu na trucksuit ya bluu bahari
- Wakati wa michezo wote watavaa trucksuit ya bluu bahari na T-shirt

viii) S i ruhusa wanafunzi wa kutwa kutembelea bwenini

ix) Si ruhusa wanafunzi wa kike kutembelea mabweni ya wanafunzi wa kiume wala wanafunzi wa kiume kutembelea mabweni ya kike

x) Wanafunzi wa kike wataruhusiwa kutoka nje ya maeneo ya shule jumamosi/jumapili ya tatu ya kila mwezi na wanafunzi wa kiume kila jumamosi/jumapili ya kwanza kila mwezi kwa ajili ya kununua mahitaji madogomadogo(shopping)

NB:Ukiukaji wa mojawapo ya sheria,kanuni na taratibu zilizoorodheshwa hapo juu waweza kumsababishia mvunjaji kuchukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

''NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA NA KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI KAFULE''

……..
DAUDI MWAKATOGA
MKUU WA SHULE

SHUKE YA SEKONDARI KAFULE
FOMU YA KUKUBALI

1.Sehemu ya mwanafunzi

Mimi……Ninaikubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha kwanza/tano……katika shule ya sekondari ya kafule na nitafika shuleni bila kuchelewa.Ninaahidi kwamba nitatii na kuzingatia sheria zote za shule na za nchi.Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za Elimu ya kujitegemea.

Anuani yangu ya kudumu ni……..

……..

……..

……..

……..

2.Sehemu ya mzazi/mlezi

Mimi…….....ninakubali mtoto wangu…….....kuchukua nafasi kuingia shule ya sekondari kafule kidato cha……..Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule.Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote na kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na Taifa.

Anuani yangu ya kudumu ni:-……..

……..

……..

……..

Iwapo nitapata uhamisho au kubadili makazi ni lazima nitaijulisha shule kwa maandishi

Saini……tarehe……

SHULE YA SEKONDARI KAFULE
TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1.Jina langu kamili lilivyotumika kidato cha nne……Dini yangu/dhehebu……..
2.Jina kamili la baba mzazi/mlezi……..kazi yake……..
Anwani kamili ya baba mzazi/mlezi……..
Namba yake ya simu ya mkononi……..
Mahali anakoishi baba mzazi/mlezi……..
Namba yake ya simu ya mezani……
Mahali anakoishi baba mzazi/mlezi:
Mkoa……Wilaya……Tarafa……kata……
Kijiji/mtaa……..
3. Jina kamili la mama mzazi/mlezi……..kazi yake……..
Anwani kamili ya mama mzazi/mlezi……..
Namba yake ya simu ya mkononi……..
Mahali anakoishi mama mzazi/mlezi……..
Namba yake ya simu ya mezani……
Mahali anakoishi mama mzazi/mlezi:
Mkoa……Wilaya……Tarafa……kata……
Kijiji/mtaa……..

4.Majina ya watu watano wanaoruhusiwa kumtembelea/kumchukua mtoto wako

Na	Jina lake	Uhusiano	Mahali anakoishi	Anuani na namba yake ya simu
01				
02				
03				
04				
05				

5.Shule nilizosoma msingi hadi kidato cha nne

Na	Jina la shule	Darasa/kidato	Kuanzia mwaka hadi mwaka	Mkoa	Wilaya	Kijiji/Mtaa
01						
02						
03						
04						
05						

Namba yangu ya Mtihani wa kidato cha nne……..

6.Matokeo yangu ya mtihani wa kidato cha nne.

Na	Somo	Daraja	Na	Somo	Daraja
01					
02					
03					
04					
05					
06					
07					
08					
09					
10					

Nilipata division……..point……..

7.Tarehe niliyoripoti hapa kafule sekondari ni……..Masomo nitakayosoma ni

1……..2……..3……..4 ……

5……..6……..

Matarajio yangu baada ya kuhitimu masomo yangu mfano kuwa Daktari,mwanasheria. N.k

1……..

2……..

3……..

Hapa shuleni ningependa nijiunge na

1.Michezo

(i)……..ii)……..iii)…….

2.Kikundi cha utamaduni wa ……..

3.Mradi wa ……

8.Taja kipaji ulichonacho na ungependa kukindeleza ……

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRIME MINISTER'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATIVE AND LOCAL GOVERNMENTS

KAFULE SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 09,
ILEJE.
……../……./20….

DISTRICT MEDICAL OFFICER
P.O.BOX……
……

Dear Sir/Madam

Re: A REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please examine……..as to his/her physical and mental fitness for admission as a form five student at Kafule secondary school in the year 2016/2017

Yours sincerely

……
HEADMASTER

The headmaster,

I have examined the student (……..) as shown below and consider that he/she is physically and mentally fit/unfit for admission to pursue a full time secondary education.

1) Vision with/without glasses,Right……left…….....
2) Blood pressure……...Haemoglobin……
3) Hearing……
4) Urine (a) Albumen……(b) Sugar……...
5) (a) Venerial diseases……(b) Bilharzia……
6) Pregnancy……
7) Neurosis……
8) Is there any abnormality of :- (a) The heart……..(b) Lungs…….....

(c)The spleen……

9)Are there any serious diseases e.g.Leprosy,epilepsy,asthma,diabetes etc……

Any comments……

Date:……..

Signature of Medical Officer

Station…… ……

Designation……..